

Na Lydia Churi-NEC

Tume ya Taifa ya uchaguzi imetaja idadi halisi ya wapiga kura katika Daftari la Kudumu la Wapiga kura kuwa ni 22,751,292 walioandikishwa na Tume hiyo na 503,193 walioandikishwa na Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC).

Akizungumza na viongozi wa vyama vya Siasa nchini, Mkurugenzi wa NEC Kailima Ramadhan alisema idadi hiyo inatokana na uhakiki na uchakataji wa taarifa za wapiga kura walioandikishwa wakati wa zoezi la uandikishaji kwa BVR.

Alisema NEC ilikamilisha uandikishaji wa wapiga kura kwa BVR Agosti 04, mwaka huu ambapo taarifa za awali za watu walioandikishwa kwenye vituo vya kuandikishia ilikuwa ni 23,782,558.

Kwa mujibu wa Kailima, Tume ilibaini kuwa wananchi 181,452 walijiandikisha zaidi ya mara moja hadi nane kwa mtu mmoja, na 845,944 walibainika kuwa ni wale waandikishaji wa 'BVR Kits' ambao jumla yao walikuwa ni 74,502 walikuwa wakifanya mazoezi ya vitendo kabla ya uandikishaji kuanza.

Mkurugenzi huyo wa NEC aliendelea kufafanua kuwa watu 3870 walioandikishwa walibainika kuwa siyo raia wa Tanzania ambapo vitambulisho vyao vimerejeshwa na taarifa zao kufutwa kwenye Kanzidata ya Daftari la Kudumu.

Aidha Kailima alisema NEC imeandaa vituo vya kupigia kura 65,105 ambapo Tanzania Bara kutakuwa na vituo 63,525 na Zanzibar ni vituo 1,580. Aliongeza kuwa kila kituo kitakuwa na uwezo wa kuhudumia wapiga kura 450 na wasiozidi 500.

Alisema kituo kitakachokuwa na wapiga kura zaidi ya 500 kitagawanywa katika vituo viwili kwa idadi sawa kwa kila kituo na kuwashauri wapiga kura kwenda katika vituo walivyojiandikishia kupiga kura siku nane (8) kabla ya siku ya kupiga kupiga kura ili kujua vituo halisi vya kupigia kura.

Aidha, wapiga kura wanaweza kupata taarifa zao zilizoko kwenye kanzidata kwa kutumia simu zao za kiganjani bila wao kulazimika kufika vituoni kwa kupiga namba *152*00 na kufuata maelekezo.

Tume imeshapokea vifaa kwa ajili uchaguzi na kuvisambaza nchi nzima. Vifaa ambavyo bado havijasambazwa ni pamoja na karatasi za kupigia kura, wino maalum, karatasi za matokeo na mihuri ya vituo. Kutokana na umuhimu wake, vifaa hivi vitasambazwa karibuni.